JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# CHAMA CHA POOL TABLE MKOA WA ARUSHA

ARUSHA POOL ALLIANCE

APA

## KATIBA

FEB,2024

# KATIBA YA CHAMA CHA
# POOL TABLE MKOA WA ARUSHA
# ARUSHA POOL ALLIANCE -APA

**Kama ilivyoandaliwa Feb, 2024**

# KATIBA CHAMA CHA POOL TABLE MKOA WA ARUSHA - ARUSHA POOL ALLIANCE -APA YA MWAKA -2024

## YALIYOMO

*Ibara* *Kichwa Cha habari na maelekezo*

## UTANGULIZI

## SURA YA KWANZA

## ARUSHA POOL ALLIANCE - APA

## SEHEMU YA KWANZA

### JINA , TAFSIRI , LENGO

**1.** **Jina la Katiba na Kuanza Kutumika**

Katiba hii itajulikana kama katiba ya Chama cha Pool Table "ARUSHA POOL ALLIANCE - APA" ya mwaka 2024 na itaanza kutumika baada ya kukubaliwa na wanachama na kuthibitiswa na mwanasheria

**2.** **Tafsiri**

"Chama"maana yake ni muungano wa wadau wote wa mchezo wa pool table Jijini Arusha (ARUSHA POOL ALLIANCE - APA).

"Viongozi" maana yake ni Mwenyekiti,Katibu, na Mweka Hazina.

"Wanachama" maana yake ni wanachama waanzilishi, wanachama wa kawaida kwa mujibu wa katiba.

## 3. Lengo

Umoja Wa Chama cha mchezo wa Pool Table ni asasi isiyo ya kiserikali yenye makao makuu yake ndani ya Jiji la ARUSHA, chama chenye lengo la kusaidia kukuza maendeleo katika mchezo wa pool table wanachama wake pamoja na taifa kwa ujumla.

# SEHEMU YA PILI

## KATIBA, ENEO LA UTENDAJI KAZI, MISINGI YA CHAMA

## 4. Jina la Chama

Jina la chama cha pool table ni ARUSHA POOL ALLIANCE - APA

## 5. Ofisi Kuu Za Chama

Ofisi kuu za chama cha pool table ARUSHA  zipo Mtaa wa Kaloleni - Mjini Kati

## 6. Eneo la Utendaji Kazi

Eneo la utendaji kazi litakuwa ndani ya Tanzania Bara.

## 7. Misingi ya Chama

Chama itafanya kazi katika misingi ya

A-  Haki,
B- Uadilifu,
C- Uwazi ,
D-Usawa,
E-Uwajibikaji,  na
F-Kujituma

# SEHEMU YA TATU

## DIRA, DHAMIRA, MADHUMUNI, UHIFADHI/ULINZI WA CHAMA.

**8.** **Dira**

Kuwa na jamii salama na yenye maendeleo endelevu katika nyanja zote za kijamii, kitamaduni, na kiuchumi.

**9.** **Malengo ya Chama**

1./ Kukuza na kudumisha ushirikiano miongoni mwa wanamchezo huu wa pool table katika kukuza vipaji vya mchezo huu wa pool table Tanzania.

2./ Kusaidiana kwenye shida na raha kama vile misiba na sherehe za wanachama wa Chama hichi cha pool table ARUSHA.

3./ Kulinda na kutetea haki za mwanachama kwa mujibu wa Katiba hii.

4./ Kutengeneza na kuendeleza timu ya Mkoa ( Northern Alliance )

5./ Kutengeneza ushindani wa Vilabu mbali mbali katika Mkoa wa Arusha na Viugaa vyake.

6./ Kuandaa Ligi ya Pool-table Mkoa

**10.** **Kutumika Sheria zinginezo za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na za Kimataifa.**

Klabu itaongozwa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu za nchi kwa kuzingatia katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, bila kuathiri sera na mikataba mbalimbali ya umoja wa mataifa ambapo Tanzania ni nchi mwanachama.

# SEHEMU YA NNE

## UANACHAMA NA AINA ZA WANACHAMA

**11 A.** **Uanachama**

Mwanachama wa Pool Table ARUSHA  lazima uwe;

**I/.** Mtanzania.
**II/.** Mdau au Mchezaji wa pool table
**III/.** Mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea.
**IV/.** Mwenye akili timamu.
**V/.** Mwenye kujua kusoma na kuandika.
**VI/.** Mwenye uwezo wa masuala ya kijamii ili kufikisha jamii malengo yake
**VII/.** Awe anakubalika na jamii
**VIII/.** Awe muaminifu
**IX/.** Awe mwadilifu

**12.** **Aina za Uanachama**

**I/. Wanachama Waanzilishi:** Hawa ni Wanachama waloshiriki kwa nguvu zao mawazo na rasilimali katika kufanikisha ndoto ya kuanzishwa kwa chama hiki.

**II/. Wanachama wa Kawaida:** Ni Wanachama ambao watajiunga baada ya kuanzishwa chama hiki.

**III/. Wanachama waheshima [Honorary members]** ni wanachama watakao teuliwa na wanachama wa Chama cha Pool Table Mkoa wa ARUSHA kwa kuzingatia mchango wao katika chama hiki. Wanachama hawa hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

## 13. Haki za Mwanachama

I/. Kuchagua au kuchaguliwa katika nafasi za uongozi.
II/.Kushiriki vikao na kupata taarifa za maamuzi ya Chama Cha Pool Table ARUSHA
III/. Kupata taarifa za maendeleo ya Chama Cha Pool Table ARUSHA
IV/. Kuhudhuria mikutano na vikao vya chama.
V/. Kupiga Kura.
VI/.Kushiriki katika shughuli mbalimbali za chama .

## 14. Kukoma Uanachama

Uanachama wa mwanachama yoyote anayetambulika na chama cha pool table mkoa wa ARUSHA utakoma kwa sababu zifuatazo;

**I./** Kifo
**II./**Amekiuka katiba ya Chama
**III./** Kuugua ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari;
**IV./** Kutoa maneno ya kichochezi,ubaguzi na lugha mbaya kwa wanachama.
**V./** Kujiondoa mwenyewe kwa ridhaa yake
**VI./**Atajihusisha na wizi wa mali za chama uchochezi wa aina yoyote kukosa nidhamu kwa Viongozi waliochaguliwa kulingana na katiba ya chama;
**VII./**Kwa kuvunja sheria za nchi ambazo zinaathiri shughuli za chama.

## 15. Kurejea Uanachama

**I/.** Mwanachama Aliyekoma uanachama kwa matatizo ya akili, atarejea uanachama kwa kuomba kwa barua endapo itathibitishwa na tabibu anayetambulika kisheria kuwa amepona.

**II/.** Uamuzi wa kurejea uanachama utaridhiwa na Mkutano mkuu wa wanachama.

## 16. Wajibu wa Mwanachama

**I./** Kuhudhuria Mikutano yote ya aina tatu (3) Mkuu, kawaida na dharula.

**II./** Kuchangia chama.

**III./** Kutunza mali za chama.

**IV./** Kutoa mawazo yake kuhusu mwenendo wa chama.

**V./** Kugombea nafasi ya uongozi

**VI./** Kuchaguliwa katika nafasi ya uongozi.

# SEHEMU YA TANO

## MUUNDO WA UONGOZI

**17.** **Mwenyekiti**

Kutakuwa na Mwenyekiti ambapo Mwenyekiti;

**I./** Atakuwa Msimamizi wa shughuli zote za chama

**II./** Atakuwa Msimamizi wa mikutano ya chama

**III./** Atakuwa ndio msemaji wa chama

**IV./** Atakuwa Msimamizi mkuu wa utendaji wa chama

**V./** Atasaini Mikataba yote ya chama

**VI/**Mwenyekiti atakuwa na jukumu la kuteua Kamati ya Mashindano akishirikiana na Katibu na Wajumbe wa tatu.

**18.** **Katibu Mtendaji**

Kutakuwa na katibu mtendaji ambaye,

**I./** Atakuwa mtendaji mkuu wa shughuli za chama

**II./** Atatunza kumbukumbu zote na mali za chama.

**III./** Kwa kushirikiana na Mwenyekiti ataitisha vikao na mikutano ya chama.

**IV./** Ataandika muhtasari wa vikao na Mikutano na kusambaza kwa wajumbe muhtasari uliopita.

**V./** Atafanya kazi yoyote atakayoelekezwa na Mkutano mkuu na chama

**VI./** Atakuwa miongoni mwa watia sahihi katika akaunti ya benki ya chama.

**VII./** Atakuwa msimamizi mkuu wa miradi yote ya chama.

**VIII./** Atakuwa mbunifu wa miradi ya chama.

**IX./** Atakuwa msimamizi na mwangalizi wa shughuli zote za miradi.

**X./** Atashirikiana na mwekahazina katika kutunisha mfuko wa chama.

**XI./** Atapitisha matumizi yote ya chama kutoka kwa wafanyakazi wa vitengo na kutia sahihi nyaraka za kibenki.

**XII./** Atandaa taarifa ya mwezi, mwaka na kuwasilisha katika mikutano ya kamati tendaji na mkutano mkuu.

## 19. Mweka-Hazina

Kutakuwa na mweka hazina ambaye,

**I./** Atatunza vitabu vya fedha na fedha zote kulingana na taratibu za fedha;

**II./** Atawajibika kutoa taarifa ya kila mwezi na mwaka ya fedha;

**III./** Atasaidiana na wakaguzi kutoka nje ya kikundi ili kuepuka hati chafu za utunzaji wa fedha;

**IV./** Atakuwa miongoni mwa watia saini benki kwa akaunti ya chama;

**V./** Atakua msimamizi wa mhasibu kwa niaba ya chama.

**VI./** Atasaidiana na katibu kuandaa taarifa ya fedha kwa ajili ya mikutano ya kamati tendaji na mkutano mkuu wa mwaka.

**VII./** Atashirikiana na katibu kutunisha mfuko wa chama.

# SEHEMU YA SITA

## UCHAGUZI WA MUDA WA KUKAA MADARAKANI

**20.** **Mwenyekiti**

Mwenyekiti atachaguliwa na Mkutano Mkuu na miongoni mwa wanachama na atakaa madarakani kwa muda wa miaka mitatu (3).

**21.** **Katibu Mtendaji**

Katibu Mtendaji atachaguliwa na Mkutano Mkuu miongoni mwa wanachama kwa kuzingatia sifa za uongozi na atakaa madarakani kwa muda wa miaka mitatu (3). Na anaweza kuchaguliwa tena kwa ridhaa ya wanachama.

**22.** **Mweka Hazina**

Mweka Hazina atachaguliwa na Mkutano Mkuu miongoni mwa wanachama kwa kuzingatia uwezo wake na elimu na atakaa madarakani kwa muda wa miaka mitatu (3). Na anaweza kuchaguliwa tena kwa ridhaa ya wanachama.

**23.** **Kuchaguliwa Tena**

Mwenyekiti, Katibu, na Mweka Hazina wanaweza kuchaguliwa tena kwa kupigiwa kura kwa kipindi kingine cha miaka mitatu kwa muhula wa pili na wanachama kama wataridhia.

# SEHEMU YA SABA

## MKUTANO MKUU

**24.** **Wajumbe Wa Mkutano Mkuu**

I./ Kutakuwa na Mkutano Mkuu ambao utakuwa chombo cha juu cha maamuzi kitakachojumuisha Wanachama wote wa Chama Cha Pool Table ARUSHA ,

II./ Maamuzi yatakuwa ni ya kura na wengi ndio watakua wameshinda.

**25.** **Wajibu: Mamlaka na kazi za Mkutano Mkuu**

I./ Kuthibitisha uteuzi wa Mkaguzi wa mahesabu;

II./ Kuchagua viongozi wa chama;

III./ Kupitia na kupitisha bajeti ya matumizi kwa kipindi husika;

IV./ Kupitia na kujadili taarifa za utekelezaji wa chama.

V./ Kujadili maendeleo ya chama;

VI./ Kufanya marekebisho ya chama;

VII./ Kuvunja chama

VIII./ Kupokea Wanachama wapya na kuondoa wanachama ;

IX./ Kujadili mapato na matumizi ya chama.

X./ Kupitisha kamati ya ushauri mpya au wajumbe wapya au kuwaondoa wajumbe kulingana na muda wa kukaa madarakani.

## 26. Kukasimu madaraka ya Mkutano Mkuu

Mkutano Mkuu unaweza kukasimu madaraka yake kwa Bodi ya kikundi. Bodi itatakiwa kutoa taarifa katika Mkutano Mkuu utakaofuata ili kuthibitisha maamuzi hayo.

## 27. Mkutano Mkuu Wa Mwaka

I./ Mkutano Mkuu wa mwaka utafanyika mara moja kwa mwaka.

II./ Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka itatolewa kwa wanachama wote kwa maandishi na kwa siku zisizopungua 21 kabla ya siku ya mkutano.

III./ Akidi ya Mkutano Mkuu wa Mwaka itakuwa ni 2/3 ya Wanachama.

## 28. Mkutano Mkuu Wa Dharura

I./Mkutano Mkuu wa Dharula utaitishwa na chama endapo kutatokea jambo la dharura ambalo linahitaji maamuzi ya Mkutano Mkuu kwa haraka;

II./Taarifa ya Mkutano mkuu wa dharula itatolewa kwa Wanachama wote kwa siku zisizopungua 5 kabla ya siku ya mkutano;

III./Akidi ya Mkutano Mkuu wa dharura wa chama itakuwa ya Wanachama wote.

## 29. Mkutano Mkuu Wa Kawaida

I./ Mkutano mkuu wa kawaida utafanyika mara tatu kwa mwaka.

II./ Taarifa ya mkutano itatolewa siku 10 kabla ya siku ya mkutano

III./ Akidi ya Mkutano itakuwa 2/3 ya Wanachama wote;

# SEHEMU YA NANE

## UTUNZAJI WA FEDHA, VYANZO VYA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA

### 30. Mwaka Wa Fedha

Mwaka wa fedha wa chama utakuwa kuanzia mwezi Januari hadi Disemba kila mwaka.

### 31. Vyanzo Vya Fedha

Vyanzo vya fedha ya chama vitakuwa ni:-

I./ Ada na viingilio vya Wanachama;

II./ Michango mbalimbali ya Wanachama

III./ Miradi mbalimbali ya uzalishaji mali;

### 32. Matumizi ya fedha za chama

Fedha zitatumika kulingana na malengo ya Chama Cha Pool Table Mkoa Wa ARUSHA.

## 33. Matumizi ya fedha za chama

**I./** Chama kitafungua akaunti katika Benki itakayoamuliwa na Wanachama wote katika Mkutano Mkuu;

**II./** Akaunti ya Benki itakuwa na watia Sahihi watatu (3) kama ifuatavyo:-

**-KUNDI A:** Wanachama watatu walichaguliwa kwenye mkutano mkuu.

**-KUNDI B:** Mweka Hazina

-**Mweka hazina** atakuwa ni mtia sahihi wa lazima pamoja na wanachama wawili kati ya wanne waliochaguliwa.

## 34. Taarifa ya Mwaka

Viongozi wataandaa Taarifa ya Mwaka itakayo jumuhisha Taarifa ya kazi na Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu na kuiwasilisha katika Mkutano Mkuu ili kuthibitisha.

# SEHEMU YA TISA

## MABADILIKO YA KATIBA NA KUVUNJA CHAMA

**35.** **Mabadiliko ya Katiba**

I./ Katiba hii inaweza kurekebishwa kama kuna ulazima kwa maamuzi ya 2/3 ya Wanachama katika Mkutano Mkuu.

II./ Taarifa ya mapendekezo ya mabadiliko ya katiba yanatakiwa kupewa wanachama siku 30 kabla ya siku ya kujadili na kupitisha mabadiliko hayo.

**36.** **Kuvunja Chama**

Klabu itavunjika endapo:-

**I./** 2/3 ya wanachama katika Mkutano Mkuu watakuwa wameafiki.

# SEHEMU YA KUMI

## UTATUZI WA MIGOGORO

**37.** **Utatuzi Wa Migogoro**

Endapo kutatokea mgogoro ndani ya Chama cha Pool Table Mkoa wa Arusha (APA), utatatuliwa kwa utaratibu ufuatao:

**38.** **Kamati ya Nidhamu**

- Kamati hii itakuwa chini ya Mwenyekiti na wajumbe walioteuliwa na Bodi ya Chama.

- ***Majukumu ya Kamati ya Nidhamu*** ni kusimamia na kufuatilia nidhamu ya mchezo ndani na nje ya uwanja kwa wachezaji na washabiki.

**39.** **Makosa ya Nidhamu**

- Mchezaji au mshabiki atakayepatikana na makosa yafuatayo atachukuliwa hatua stahiki:

  - Kutoa lugha za matusi
  - Kuchochea vurugu wakati wa mchezo
  - Ushangiliaji usio wa kistaarabu kipindi cha mchezo ukiendelea
  - Kutoa lugha za kibaguzi au maneno yanayogawa watu
  - Matendo yote yasiyofaa kwenye mchezo

## 40. Hatua za Nidhamu

- Kamati ya Nidhamu inaweza kuchukua hatua zifuatazo kulingana na uzito wa kosa lililofanywa:

- **Kuonywa:** Onyo rasmi kwa mchezaji au mshabiki husika.

- **Kupigwa faini:** Kuweka adhabu ya kifedha kwa mchezaji au mshabiki.

- **Kufungiwa kucheza:** Kumfungia mchezaji asishiriki katika michezo kadhaa au yote ya mashindano.

- **Kuondolewa kwenye mashindano:** Kumwondoa mchezaji au mshabiki kutoka kwenye mashindano kwa muda au kabisa.

- **Kubatilishiwa matokeo:** Kubatilisha matokeo yaliyopatikana kwa mchezaji au timu endapo utovu wa nidhamu umeathiri mchezo.

- **Kushitakiwa:** Kuchukua hatua za kisheria endapo kosa ni la jinai au linakiuka sheria za nchi.

Ikiwa mgogoro huo hautatatuliwa na Kamati ya Nidhamu, basi utapelekwa kwa Bodi ya Chama. Endapo Bodi itashindwa kutatua mgogoro huo, mkutano mkuu wa wanachama utaamua hatua za kuchukua.

## 41. Utekelezaji

- Kamati ya Nidhamu itawajibika kutoa taarifa za mara kwa mara kwa Bodi juu ya masuala ya nidhamu yanayojitokeza.

- Vikao vya Kamati ya Nidhamu vitafanyika mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa nidhamu inazingatiwa wakati wote wa mashindano.

## 42. Hitimisho

Utekelezaji mzuri wa sheria na kanuni hizi utahakikisha kuwa michezo inachezwa kwa amani na utulivu, na hivyo kukuza mchezo wa pool table katika Mkoa wa Arusha na kwingineko.

## 43. Marejeo ya Rasimu ya APA

- Kamati ya Nidhamu itafuatilia na kusimamia nidhamu ya mchezo kwa ujumla ikiwa ni ndani na nje ya mchezo kwa mazingira ya uchezaji na ushangiliaji.

## WAJUMBE KWA PAMOJA KWA MAJINA NA SAHII WAMEPITISHA RASIMU HII KUWA KATIBA YA CHAMA CHA POOL TABLE ARUSHA- APA

| NO | MAJINA MATATU | SAHIHI |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

## WAJUMBE KWA PAMOJA KWA MAJINA NA SAHII WAMEPITISHA RASIMU HII KUWA KATIBA YA CHAMA CHA POOL TABLE ARUSHA- APA

| NO | MAJINA MATATU | SAHIHI |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

## WAJUMBE KWA PAMOJA KWA MAJINA NA SAHII WAMEPITISHA RASIMU HII KUWA KATIBA YA CHAMA CHA POOL TABLE ARUSHA- APA

| NO | MAJINA MATATU | SAHIHI |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# CHAMA CHA POOL TABLE MKOA WA ARUSHA

## RASIMU YA KATIBA

FEB,2024